# Ujumuishaji wa Tafakuri Tunduizi katika Mitihani ya Taifa ya Shule za Sekondari Nchini Rwanda: Mfano wa Kiswahili Kidato cha Sita

*JLLE*
Vol 18(1) 1–17
© The Publisher
DOI:10.56279/jlle.v18i1.1

*Laurien Tuyishimire*[1]
**ORCID:** 0009-0001-0530-4607
and
*Donard Bikorimana*
**ORCID:** 0000-0002-3689-4945

**Ikisiri**

*Tafakuri tunduizi inawawezesha wanafunzi wa lugha kufanya kazi kwa ufanisi kuzidi wanafunzi wengine ambao hawakuikuza. Hii inatokana na kwamba wanafunzi wenye stadi hii huwa na uwezo wa kufikiri kihakiki kuhusu masuala yanayohusiana na mazingira ya kazi na maisha kwa ujumla. Pamoja na hayo, fasihi inachukuliwa kama nyenzo ya kukuza stadi za tafakuri tunduizi kutokana na uchangamano wa vipengele vyake. Hivyo basi, makala yetu inalenga kujadili ujumuishaji wa stadi za tafakuri tunduizi katika mitihani ya Kiswahili ya taifa kwa shule za sekondari nchini Rwanda. Kupitia uchambuzi wa mitihani ya taifa ya somo la Kiswahili na matini mbalimbali kuhusu tathmini ya tafakuri tunduizi, tumebaini kwamba stadi za tafakuri tunduizi hazijumuishwi kwa ufanisi katika mitihani ya taifa ya somo la Kiswahili hasa katika kipengele cha fasihi. Baadhi ya maswali ya mtihani hayawapi wanafunzi uhuru wa kuhusisha hali ya darasani na maisha halisi ya utatuzi wa matatizo. Kwa hivyo, makala imetoa mikakati inayopaswa kuzingatiwa ili kuandaa maswali ya mitihani ya lugha ya Kiswahili kwa kujumuisha tafakuri tunduizi ipasavyo. Baadhi ya mikakati hiyo ni pamoja na kuzingatia malengo na mahitaji ya mwanafunzi na yale ya mtaala tumizi, kuhakikisha kuwa mwanafunzi anapewa fursa ya kuzalisha mawazo mapya kama matokeo ya ujifunzaji na kuandaa maswali ya mtihani yanayoakisi mazingira halisi ya utatuzi wa matatizo.*

**Maneno Msingi:** *Stadi za tafakuri tunduizi, tathmini, mtihani wa taifa, fasihi*

**Abstract**

*Language students with critical thinking are able to perform activities that other students cannot. This is because they are able to think critically about issues related to the workplace and life in generally. Literature is considered as a tool for developing critical thinking due to the complexity of its elements. Therefore, the main purpose of this paper is to analyse the integration of critical thinking skills in secondary-school national examinations in Rwanda. Through analysis of Kiswahili*

[1] **Corresponding author:**
Laurien Tuyishimire, Department of Humanities and Language Education, University of Rwanda, Kigali, Rwanda. E-mail: l.tuyishimire@ur.ac.rw

*national examinations and various literature reviews about assessment of critical thinking, we have identified that critical thinking skills are not well integrated into the secondary-school Kiswahili national examinations in Rwanda, especially in the literature component. Some examination questions do not reach the level of requiring students to relate the classroom situation to real-life problem-solving. Therefore, the article suggests strategies to integrate critical thinking skills when preparing Kiswahili the examinations . Some of those strategies include considering the goals and needs of the students and those of the relevant curriculum, ensuring that student can generate new ideas as a result of learning, and preparing examination questions that reflect the real-word problem-solving context.*

**Keywords:** *Critical thinking skills, assessment, national examination, literature*


**Utangulizi**

Mnamo mwaka wa 2015, Wizara ya Elimu nchini Rwanda ilianza kutekeleza mtaala mpya unaorejelewa kama mtaala unaoegemea uwezo. Mtaala huu unazingatia zaidi mahitaji ya mwanafunzi na kumfanya awe na uwezo wa kutekeleza yale anayojifunza darasani katika muktadha wa maisha halisi. Hivyo, ataweza kushindana kwenye soko la ajira kitaifa na kimataifa (REB, 2015). Kutokana na mtaala huu, ufundishaji wa tafakuri tunduizi unapaswa kufanyika ndani ya kila somo linalofundishwa (Nsengimana, 2021).

Shirkhani na Fahim (2011) wanatanabahisha kwamba ufundishaji wa tafakuri tunduizi katika madarasa ya lugha huwasaidia wanafunzi kuwa na matokeo mazuri darasani na kuwawezesha kufanya kazi kwa ufanisi kuzidi wanafunzi wengine ambao hawakukuza. Chanzo cha ufanisi huu huwa ni uwezo wa kufikiri kihakiki kuhusu masuala yanayohusiana na mazingira ya kazi na maisha kwa ujumla. Aidha, wanafunzi wenye tafakuri tunduizi huwa na uwezo wa juu wa kiudadisi ili kugundua tatizo na kulitolea majibu (Belecina & Ocampo, 2018). Kwa hiyo, kuwaandaa wanafunzi wenye uwezo wa kukabiliana na matatizo mbalimbali ya kimaisha na kuweza kushindana kwenye soko la ajira katika zama hizi ambapo tunategemea ufundishaji mwafaka wa tafakuri tunduizi.

Rezaei, Derakhshan na Bagherkazemi (2011) wanaelezea kwamba mojawapo ya mikakati ya kufundisha tafakuri tunduizi ni pamoja na tathmini yake. Wanafunzi wanalazimika kufanyiwa tathmini ili ujifunzaji ukamilike (Alsaleh, 2020). Hivyo basi, tathmini inapaswa kuanzia kwa kile mwanafunzi anakumbuka hadi kile anaweza kuunda mwenyewe kama matokeo ya ujifunzaji wake.

Hoja hii inaungwa mkono na Mamlaka ya Taifa ya Ukaguzi wa Mitihani na Shule nchini Rwanda (NESA). NESA (2022) inatoa sharti kwamba mtihani unapaswa kuandaliwa kwa kuzingatia grafu ya Taksonomia ya Bloom. Ni lazima maswali mengi yaweke mkazo kwenye ngazi za chini kwa kiwango cha asilimia 70. Aidha, asilimia 30 ya mtihani iwe maswali ya kiwango cha juu cha tafakuri tunduizi. Maswali haya huwawezesha wanafunzi kuchambua, kutathmini na kuunda kama inavyoonekana kwenye kielelezo hapa chini.




**Chanzo:** NESA (2022)

Grafu hii na asilimia zake inaonesha wazi kwamba ngazi za chini (*kukumbuka, kuelewa* na *kutumia*) zinapaswa kutiliwa mkazo zaidi kwa sababu ndio msingi wa mwanafunzi kuweza kutekeleza stadi za tafakuri tunduizi ambazo ni *kuchambua, kutathmini* na *kuunda* (Krathwohl, 2001 katika Van Der Zanden, Denessen, Cillessen & Meijer, 2020). Hata hivyo, tafiti zinaonesha kwamba walimu wanashindwa kufundisha na kutathmini tafakuri tunduizi kwa ufanisi. Hii inatokana na kwamba wanaandaa tathmini zenye maswali yanayowataka wanafunzi kurudisha kile walichokariri kichwani kuliko kuwasaidia kuhusisha kile walichosoma na maisha halisi (Tuyishimire & Mlaga, 2023). Athari yake ni kuwa na wanafunzi wanaomaliza shule za sekondari na vyuo vikuu wakiwa na kiwango cha chini cha tafakuri tunduizi na hivyo wanashindwa kutoa mchango wao kimaendeleo (Schendel, 2015).

Hali hii imetutia hamasa ya kuchunguza namna stadi za tafakuri tunduizi zinavyojumuishwa katika mitihani ya taifa ya wanafunzi wa kidato cha sita katika shule za sekondari nchini Rwanda. Pamoja na hayo, makala yetu imejikita katika kipengele cha fasihi tu. Hii inatokana na kwamba fasihi inachukuliwa kama nyenzo mwafaka ya kukuza tafakuri tunduizi miongoni kwa wanafunzi (Sidhu, Fook & Kaur, 2010). Wataalamu hawa wanatanabahisha kuwa kupitia mjadala wa vipengele vya kazi ya kifasihi ambavyo ni dhamira, thamani na mitazamo huwapa wanafunzi fursa ya kukuza stadi za tafakuri tunduizi kutokana na uchangamano wake.

Aidha, Tung na Chang (2009) wanaongezea kwamba kupitia mada inayozungumziwa, mawanda na lugha ya kazi husika ya kifasihi huwasaidia msomaji au msikilizaji kujenga maana za kibnafsi na kimaisha. Hivyo, anaweza kutathmini matendo ya wahusika kadri wanavyoingiliana na mazingira yao na kuweza kubaini sababu zinazowafanya kuwa na mienendo tofauti. Kwa namna hiyo, makala yetu ina malengo mawili: Mosi, kujadili namna stadi za tafakuri tunduizi zinavyojumuishwa katika mitihani ya taifa ya somo la Kiswahili hususan katika kipengele cha fasihi. Pili, kupendekeza mikakati ya kuandaa tathmini inayojumuisha stadi za tafakuri tunduizi katika somo la Kiswahili. Kabla ya kutoa maelezo zaidi, ni muhimu kuzungumzia methodolojia na nadharia iliyoongoza utafiti huu.

**Methodolojia na Nadharia ya Utafiti**

Data za makala hii zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa matini. Hii ni mbinu inayomsaidia mtafiti kupata data za utafiti ambazo zimerekodiwa bila kumhusisha mtafiti, data hizi zinajumuisha maneno na taswira (Silverman na Marvast, 2008). Hivyo basi, katika uchambuzi wa matini, kwa kiwango kikubwa tumechambua mitihani ya taifa ya somo la Kiswahili na matini mbalimbali kuhusu tathmini ya tafakuri tunduizi ili kufanikisha malengo ya utafiti wetu kama yalivyobainishwa. Uchambuzi wa mitihani ya taifa ulitupa picha kuhusu namna stadi za tafakuri tunduizi zinavyojumuishwa katika mitihani ya taifa hususan katika kipengele cha fasihi. Vilevile, mbinu ya uchambuzi wa matini kuhusu tafiti tangulizi imetufaa kupendekeza mikakati ya kuandaa tathmini inayojumuisha stadi za tafakuri tunduizi katika somo la Kiswahili.

Licha ya Kiswahili kufundishwa kuanzia kidato cha kwanza hadi kidato cha sita katika shule za sekondari nchini Rwanda, Kiswahili hutahiniwa katika mitihani ya taifa ya wanafunzi wa kidato cha sita. Pia, fasihi huanza kufundishwa kutoka kidato cha nne hadi cha sita. Pamoja na hayo, wanafunzi wanaoshinda vizuri mtihani wa kidato cha sita hujiunga na vyuo vikuu huku wengine wakienda kutafuta ajira katika taasisi mbalimbali. Hakika, mitihani ya kidato hiki imetupa picha halisi ya namna tafakuri tunduizi inavyojumuishwa katika tathmini kwa lengo la kuwaandaa wahitimu kwa ajili ya maisha halisi.

Zaidi ya mtihani wa taifa kuwa na vipengele vinne ambavyo ni *ufahamu* wenye asilimia 15; sarufi yenye asilimia 15 pia na *utungaji* ulio na asilimia 30 pamoja na *fasihi katika Kiswahili* ambayo huwa na asilimia 40, kipengele cha fasihi ndicho kilicho na asilimia kubwa kuliko vipengele vingine kama inavyodhihirika (REB, 2015). Hii ni ithibati kwamba fasihi ni muhimu kwa wanafunzi wa lugha na ndiyo sababu inapewa uzito katika mtihani.

Mitihani iliyochambuliwa ni ile iliyofanywa kutoka mwaka wa 2018 hadi mwaka wa 2023. Tulichukua kipindi hiki kwa sababu, mwaka wa 2018 ndipo mtihani wa kwanza wa taifa wa mtaala unaoegemea uwezo ulifanyika (REB, 2015a). Aidha, hakuna mtihani wa taifa uliofanyika katika mwaka wa 2020 kutokana na janga la UVIKO 19 ambalo lilisababisha kufungwa kwa shule nchini Rwanda kutoka tarehe 15 Machi hadi Novemba, 2020 (Ndayambaje, Kamanzi, Murereyimana, Ntahomvukiye & Otara, 2023). Kwa hiyo, jumla ya mitihani iliyochambuliwa ni mitano (5).

Vilevile, data za makala hii zimechanganuliwa kwa kujiegemeza katika ruwaza ya dhamira zilizokuwa zinajitokeza katika data hizo. Tena, matokeo ya utafiti wetu yamewasilishwa kwa kujiegemeza katika ruwaza za dhamira zilizodhihirika katika uchambuzi wa data.

Kwa upande wa nadharia, utafiti wetu uliongozwa na Nadharia ya Taksonomia ya Bloom iliyoasisiwa na Benjamin Bloom mnamo mwaka wa 1956. Katika mwaka wa 2001 Taksonomia ya Bloom ilisasishwa kulingana na mahitaji ya mtaala na mfumo wa elimu ya kisasa (Chandio, Pandhiani, & Iqbal, 2016). Kulingana na mabadiliko hayo, mwanafunzi wa kiwango chochote kile anatarajiwa kutathminiwa uwezo wake kutoka ngazi ya kukumbuka hadi ngazi ya kuzalisha mawazo mapya au kitu kipya (kuunda). Hivyo, tathmini inabidi kujumuisha maswali yanayopima uwezo wa mwanafunzi wa kutenda au kuzalisha hoja mpya zinazoweza kutumiwa kutatua matatizo kwa kutumia ujuzi alionao (Chandio na wenzake, 2016).

Pamoja na hayo, utafiti wetu umeongozwa na mihimili ifuatayo: Mosi, ufundishaji na tathmini zinapaswa kujumuisha vikoa vitatu. Hivyo ni kikoa cha utambuzi, uathiriaji na kikoa cha kiakili-matendo. Mhimili huu umetufaa kuchuguza namna maswali yanayotolewa katika mtihani yanavyowashirikisha wanafunzi kukuza stadi za tafakuri tunduizi ambazo ni kuchambua, kutathmini na kuunda.

Mhimili wa pili ni ufundishaji na tathmini ambazo zinapaswa kujumuisha ngazi zote za upimaji au tathmini kutoka ngazi za chini hadi ngazi za juu. Mhimili huu umetuwezesha kuchunguza ikiwa maswali ya tathmini yanaanzia ngazi za chini (kukumbuka) hadi ngazi za juu (kuunda). Kwetu, hii imekuwa pia fursa ya kutoa mapendekezo kuhusu namna mitihani ingeandaliwa kwa kujumuisha stadi za tafakuri tunduizi. Hii imetoa pia fursa kwetu ya kutoa mapendekezo kuhusu namna mitihani inayopaswa kuandaliwa kwa kujumuisha tafakuri tunduizi.

**Matokeo ya Utafiti**

Sehemu hii inahusu matokeo ya utafiti. Inashughulika na data za uchambuzi wa matini zilizochangia kufanikisha malengo ya utafiti. Kama ilivyofafanuliwa hapo awali, malengo hayo ni haya yafuatayo: Kujadili namna stadi za tafakuri tunduizi zinavyojumuishwa katika mitihani ya taifa ya somo la Kiswahili hususan katika kipengele cha fasihi na kupendekeza mikakati ya kuandaa tathmini inayojumuisha stadi za tafakuri tunduizi katika somo la Kiswahili. Kwa hiyo, kwa lengo la kwanza, tumefanya uchambuzi wa mitihani ya taifa kwa kuangalia namna stadi za tafakuri tunduizi zinavyojumuishwa katika kipengele cha fasihi. Kwa lengo la pili, tumepitia tafiti mbalimbali zilizotangulia ili tupendekeze mikakati ya kuunda tathmini kwa kujumuisha stadi za tafakuri tunduizi.

**Ujumuishaji wa Stadi za Tafakuri Tunduizi katika Mitihani ya Taifa**

Data za uchambuzi wa matini zinaonesha kwamba aghalabu mitihani ya Kiswahili katika kiwango cha taifa iliandaliwa kwa kuzingatia grafu ya Taksonomia ya Bloom. Maswali mengi hupaswa kuweka mkazo kwenye ngazi cha chini ambazo ni *kukumbuka, kuelewa* na *kutumia*. Hata hivyo, stadi za juu za tafakuri tunduizi zinazomlazimisha mwanafunzi kuzalisha hoja mpya kutokana na ujuzi walionao hazikuzingatiwa kwa ufanisi. Jambo hili limejitokeza katika mitihani iliyochambuliwa. Kama inavyooneshwa hapo chini, tulifanya uchunguzi wa suala hili kwa kuanzia kwenye mtihani wa taifa wa Kiswahili ambao ulifanywa katika mwaka wa 2018.

**SEHEMU YA III: FASIHI (Alama 25)**

16) Eleza methali zifuatazo na utoe mfano wa hali tunapoweza kutumia kila moja: (alama 6)

(a) Usitukane wakunga na uzazi ungalipo

(b) Dalili ya mvua ni mawingu

(c) Usiache mbachao kwa msala upitao

17) Jadili vipengele vitatu kuhusu ulinganifu wa fasihi simulizi na fasihi andishi. (alama 6)

18) Kwa kutoa mifano kadhaa, eleza namna fasihi inavyoweza kuelimisha jamii. (alama 5)

19) Soma shairi hapa chini, kisha ujibu maswali yanayohusu uchambuzi wake. (alama 6)

Lugha yangu ya utoto, hata leo nimekua,
Tangu ulimi mzito, sasa kusema najua,
Sawa na manukato, moyoni mwangu na pua,
Pori, bahari na mto, napita nikitumia,
Titi la mama litamu, jingine halishi hamu.

Sababu ya kupenda, lafidhi yangu natoa,
Natumia toka ganda, na kiini chanelea,
Lugha nyingine nakonda, wakati nikitumia,
Mbele nikitaka kwenda, ulimi wangu hukwaa,
Titi la mama litamu, jingine halishi tamu.

Ujira mwema napewa, kwa lugha za kigeni,
Na bidii natoa, nyingi nisiwekwe chini,
Lakini juu ya hayo, nawaza mwangu moyoni,
Mwasi wa kutumia, lugha yake maskini,
Titi la mama litamu, jingine halishi hamu.

**REB 2018** Ukurasa wa 6 kwa 8

Chambua shairi hili kwa kueleza na kutoa mifano kutoka shairini ya sifa za kimtindo zifuatazo :

(a) Mishororo katika beti

(b) Beti

(c) Urari wa mizani

20) Tegua vitendawili vifuatavyo: (Alama 2)

(a) Kila niendapo ananifuata:

(b) Nyumba yangu haina mlango:

**Chanzo:** Data za Utafiti (2023)

Maswali ya mtihani huu ni mazuri kutokana na kwamba yanazingatia taarifa za msingi kuhusu fasihi na yanawalazimu wanafunzi kutoa maelezo na mifano mbalimbali ili kutetea majibu yao. Mifano dhahiri ioneshayo viwango hivyo ni swali la 16. Hali kadhalika, swali la 17 na 18 pia ni maswali mazuri yanayowasaidia wanafunzi kukuza stadi za tafakuri tunduizi. Pamoja na uzuri huu, tuna maoni kwamba ingekuwa bora zaidi kubainisha wazi kwamba mifano itakayotolewa na wanafunzi itatoka katika kazi za kifasihi walizosoma au kusikiliza. Kwa kufanya namna hii, wanafunzi wangepata fursa ya kuhusisha kile wamesoma/ kusikiliza katika kazi za kifasihi na maisha halisi.

Pamoja na hayo, swali la 19 hata kama linawalazimu wanafunzi kuchambua shairi, linaishia kwa kutathmini ujuzi wa kiwango cha uelewa tu (*eleza*). Hapa mwanafunzi anatarajiwa kuelewa istilahi zilizotajwa tu ili kuzitafutia mifano katika shairi.

Kwa maoni yetu, swali hili moja halitoshi. Ingekuwa bora zaidi kuongeza maswali yanayomlazimu mwanafunzi kuunda au kuendeleza shairi kwa kufuata sifa za shairi analosoma. Kwa kufanya hivi, wanafunzi wangenufaika kwa namna mbili. Mosi, kukuza uwezo wao wa kitafakuri ambao ni kuchambua, kutathmini na kuunda . Pili, kuendeleza kipaji chao cha utungaji na hivyo wanaweza kutumia fursa hii kwa ajili ya kujiendeleza kimaisha na kiuchumi. Ndio maana mtaala unaoegemea uwezo ulianzishwa kwa madhumuni ya kumpa mwanafunzi uwezo unaohitajika ili aweze kuweka vitendoni yale

anayojifunza shuleni katika hali halisi ya maisha yake ili aweze kukabiliana na changamoto yeyote inayoweza kumbalili (REB, 2015a).

Swali la 20 linahusiana na vitendawili. Vitendawili ni aina ya mafumbo yanayoficha jibu na kutolewa kama kauli au swali ili lifumbuliwe na mteguaji (Okpewho, 1992 katika Ngonyani, 2005). Kila jamii hutunga vitendawili vyake kulingana na vigezo vya kimaisha, kihali na kimazingira. Pia, vitendawili hutarajiwa kutumika kwa mtu asiyejua jibu ili achakate mazingira ya jamii, maisha na hali yake na atafute jibu mwafaka. Hivyo basi, swali la 20 ni zuri kwa madhali linamlazimu mwanafunzi kukumbuka kile alichosoma darasani. Pamoja na uzuri huu, tuna maoni kwamba wanafunzi wangeulizwa pia kujadili (*kuchambua*) umuhimu wa vitendawili katika maisha ya kila siku kuliko kuishia kutegua vitendawili vile tu.

Kutokana na hali halisi ya mtihani huu ni dhahiri shahiri kwamba mtihani unafuata vigezo vya tathmini kama vinavyotolewa na NESA ingawa sio kwa asilimia 100. Huenda ilitokana na kwamba ilikuwa mara ya kwanza wanafunzi kufanya mtihani wa mtaala mpya. Hali hii ilituhamasisha kuchunguza mtihani wa mwaka wa 2019 ili tujue na kuona hali ilivyo ukilinganisha na mtihani uliotangulia.

**REB** 2019 028 - Ukurasa wa **5** kwa **8**

**SEHEMU YA III: FASIHI (alama 25)**

18) Eleza methali zifuatazo na utoe hali tunapoweza kutumia kila moja **(alama 6)**

(a) Ukistaajabu ya Mussa utaona ya Firauni

(b) Patiliza udongo ungali maji.

(c) Ng'ombe akivunjika guu malishoni hurudi zizini kusaidiwa.

19) Kwa kutoa mifano kadhaa, eleza namna fasihi inavyoweza kuburudisha jamii. **(alama 5)**

20) Andika methali yoyote inayoelimisha watu kutoa malezi bora. **(alama 3)**

21) Toa mfano wa riwaya uliyojifunza na muhtasari wake katika mistari kati ya 7 na 10. **(alama 6)**

22) Fani na maudhui havitengani bali hutegemeana ili kazi ya fasihi iweze kuwa bora zaidi. Jadili **(alama 5)**

**Chanzo:** Data za Utafiti (2023)

Kwa kuchunguza mtihani huu, tuliona kwamba maswali yake ni mazuri. Hii ni kwa kuwa yanajumuisha maarifa mbalimbali kuhusu kile mwanafunzi anachojifunza kuhusu fasihi. Pamoja na hayo, mtihani huu unaundwa na maswali yanayohusiana kimuundo na mtihani uliofanywa katika mwaka wa 2018. Kwa mfano, swali la 18 la mtihani wa 2019 linahusiana na swali la 16 la mtihani wa 2018. Aidha, swali la 19 la mtihani wa 2019 lina uhusiano wa karibu na swali la 18 la mtihani wa 2018. Maoni yetu kuhusu maswali haya yameshajadiliwa katika uchambuzi wetu wa mtihani wa 2018.

Swali la 20, ni swali zuri linalomhitaji mwanafunzi kukuza stadi za tafakuri tunduizi kwa kiwango cha *kuchambua* na *kutathmini* anapotunga methali isipokuwa swali hili halikutolewa kwa ubayana. Vilevile, mwanafunzi hakupewa nafasi ya kutetea hoja yake

baada ya kutoa methali hiyo. REB (2015a) inaeleza kwamba swali la mtihani linapaswa kueleweka kwa ubayana. Kwa mtazamo wetu, mwanafunzi angeombwa kutoa methali akiambatanisha maelezo na mifano ya kutetea jibu lake. Kwa kufanya kwa namna hiyo, mwanafunzi angepata fursa ya kuchambua na kutathmini hoja zake wakati wa kujibu swali hili.

Zaidi ya hayo, swali la 21 nalo linamsaidia mwanafunzi kukumbuka maarifa aliyosoma katika kazi ya kifasihi na kuyazungumzia kwa machache. Licha ya umuhimu wake, swali hili ambalo linauliza muhtasari wa riwaya halimsaidii mwanafunzi kukuza stadi za tafakuri tunduizi kwa sababu muhtasari huo unaotakiwa si kazi asilia yake. Kwa hiyo, ingekuwa bora swali hili kuulizwa kwa namna ya kumtaka mwanafunzi kuhusisha kile alichosoma katika riwaya na muktadha wa maisha yake halisi ama maisha ya binadamu kwa ujumla. Hapo, mwanafunzi angeulizwa kujibu mojawapo ya maswali ya kumsaidia kukuza tafakuri tunduizi kwa kiwango cha kutathmini na kuunda. Tuyishimire na Mlaga (2021) wanapendekeza maswali yanayoweza kutolewa kwa wanafunzi kutokana na kazi ya kifasihi waliyosoma na kuwashirikisha kutoa mawazo yao wenyewe.

Baadhi ya maswali hayo ni haya yafuatayo: a) Jadili sababu za kuipenda au kuichukia kazi ya fasihi uliyosoma. (b) Bainisha na kueleza kwa nini sehemu fulani ya kazi unaipenda. (ch) Eleza funzo lililopo katika kazi husika na namna linavyokusaidia katika maisha yako. (d) Eleza ikiwa unakubaliana na mienendo ya mhusika mkuu wa kazi hiyo na eleza ni kwa nini unakubaliana nayo au la. (e) Tuseme kwamba kazi ambayo umeisoma haikufika mwisho wake. Ifikishe mwishoni kwa aya zisizopungua tatu.

Kwa ukweli, maswali kama haya yangemlazimisha mwanafunzi kutoa muhtasari wa riwaya aliyosoma ili anapojibu na fursa kwake kuboresha stadi za tafakuri tunduizi ambazo ni kuchambua, kutathmini na kuunda.

Kadhalika, swali la 22 ambalo ni la mwisho katika mtihani huu linatathmini tafakuri tunduizi kwa kiwango cha kuchambua. Pamoja na uzuri huu, ingekuwa bora kama swali lili hili likiwa wazi zaidi kwa wanafunzi na kuwalazimu kutoa mifano kutoka kazi za kifasihi ambazo waliwahi kusoma. Iwapo maswali yangetengenezwa namna hii, yangewasaidia mno wanafunzi kujenga hoja ambazo zingethibitishwa na mifano kutoka kazi za kifasihi walizosoma au kusikiliza. Hata hivyo, swali la 18 lihusulo methali na lile la 21 la kubainisha riwaya na muhtasari wake yalipewa alama nyingi ingawa si kiini cha mtihani huu.

Kwa ujumla, mtihani huu wa mwaka wa 2019 ulikuwa mzuri kwa kuwa ulizingatia grafu ya Taksonomia ya Bloom ambayo inaongoza kuiandaa mtihani. Pamoja na hayo, tuna maoni kwamba ingekuwa bora zaidi iwapo mtahini kwanza angefanya jedwali la mgawanyo wa maswali kabla ya kutengeneza mtihani ili mada zote zitathminiwe vilivyo. NESA (2022) inapandekeza kwamba kabla ya kuandaa mtihani wowote, ni lazima mtahini atengeneze mgawanyo wa maswali ili umuongoze kuandaa na kutoa alama kwa kila swali kulingana na uzito wake. Aidha, mgawanyo wa maswali humsaidia mtahini kubainisha idadi ya maswali kwa kila mada na alama zinazopaswa kutolewa kwa kila ngazi ya grafu ya taksonomia ya Bloom (kukumbuka hadi kuunda). Kwa hiyo, mtahini analazimika kuhakikisha kwamba ametumia vitenzi tendaji vinavyoonesha wazi nini mwanafunzi anatarajiwa kufanya. Baadhi ya vitenzi hivyo ni kuchambua, kutetea, kutengeneza, kulinganisha, kupendekeza, kulinganisha na kulinganua, kutetea, kubuni, kusanifu na kutofautisha tukitaja kwa uchache (REB, 2015a).

Vilevile mtihani wa mwaka wa 2020-2021 ulichambuliwa. Kama ilivyoelezwa katika sehemu ya methodolojia, katika mwaka wa 2020, hakuna mtihani uliofanywa kwa sababu ya janga la UVIKO 19 uliosababisha kufungwa kwa shule nchini Rwanda (Ndayambaje na wenzake, 2023). Mtihani ulifanywa tena katika mwaka wa masomo wa 2020-2021.

**SEHEMU YA III: FASIHI** **(alama 25)**

16) Eleza methali zifuatazo na utoe hali tunapoweza kutumia kila moja : **(alama 6)**

(a) Ngoma ikilia sana hupasuka kiwambo.

(b) Hayawi hayawi huwa.

(c) Kidole kimoja hakivunji chawa.

17) Eleza maana ya maudhui katika kazi ya fasihi kwa kutoa mfano. **(alama 4)**

18) Eleza angalau vipengele 2 vya fasihi andishi. **(alama 4)**

19) Eleza nahau zifuatazo kisha utoe mfano wa kila moja katika sentensi : **(alama 6)**

(a) Kukata ini

(b) Kupiga marufuku

(20) Chambua shairi hili kwa kueleza na kutoa mifano kutoka shairini ya sifa za kimtindo zifuatazo : **(alama 5)**

(a) Ukwapi na Utao

(b) Vina

Ajali si jambo bora, kutukia kwa yeyote,
Huathiri mara, jamii na watu wote,
Hebu wacha masihara, sijesakamwa na mate,
Dereva kuwa makini, mbona watuhatarisha,

Ajali nyingi hujiri, kwa uso mwangalifu,
Mtu hataki kukiri, ulevi naye ni kufu,
Yualipeleka gari, na mawazo yako dufu,
Dereva kuwa makini, mbona watuhatarisha,

Umepata dereva, gari kupeleka kasi,
Ngadhani mambo haiva, ahera pamoja nasi,
Kaonyesha udereva, kuvuma kwa pepo kusi,
Dereva kuwa makini, mbona watuhatarisha.

NESA 2020-2021 028 – Ukurasa wa 5 kwa 8

**Chanzo:** Data za Utafiti, 2023

Mtihani huu ni mzuri kwa sababu unazingatia baadhi ya vipengele vinavyozungumziwa katika kipengele cha fasihi. Aidha, mtihani wenyewe unaweka mkazo zaidi katika maarifa kuhusu fasihi. Haya ni msingi kwa mwanafunzi kwa vile ni chanzo cha kukuza stadi za tafakuri tunduizi. Kama ilivyojitokeza katika mitihani iliyotangulia, kuna maswali yanayofanana kimuundo. Mfano ni swali la 16 ambalo linafanana kimuundo na swali la 16 la mtihani wa mwaka wa 2018. Pia, swali jingine ni lile la 18 la mtihani wa mwaka wa 2019. Maelezo zaidi yameshatolewa kwa mitihani iliyochambuliwa.

Licha ya hayo, swali la 17, 18 na 19 ni maswali mazuri kwa sababu yanawalazimu wanafunzi kutoa maelezo (*kuelewa*) wanapojibu. Pamoja na uzuri huu, tuna maoni kwamba swali la 17 na 18 yangekuwa bayana na kuwataka wanafunzi kutoa mifano kutoka kazi za kifasihi walizosoma. Hii ingewasaidia kujenga hoja na kuzitetea kwa mifano halisi. Kwa kuongezea, swali la 17, lingebainisha wazi pia aina ya fasihi ikiwa ni fasihi andishi au simulizi.

Pia, swali la 19 ni zuri kwa sababu linamlazimu mwanafunzi kutoa maelezo na mifano kuhusu nahau zinazotolewa. Licha ya uzuri huu, tuna maoni kwamba swali lingepiga hatua zaidi na kumtaka wanafunzi kuhusisha nahau hizi na maisha halisi zinamotumiwa.

Vilevile, swali la 20 ni zuri kwa kuwa linakuza kiwango cha kuchambua. Maelezo kuhusu swali hili yametolewa katika uchambuzi wa mtihani wa mwaka wa 2018. Kwa hiyo hakuna haja ya kuyarudia ili kuepukana na uradidi.

Kama ilivyoelezwa, mtihani huu ni mzuri kwa sababu unazungumzia dhana za msingi katika fasihi ambazo zinamsaidia mwanafunzi kuboresha tafakuri tunduizi. Hata hivyo, ngazi za juu zinazomsaidia mwanafunzi kuchambua, kutathmini na kuunda hazikutiliwa mkazo kwa ufanisi wake. Baadhi ya maswali hayaoneshi wazi nini mwanafunzi anaweza kufanya kulingana na kile anachoelewa kwa ajili ya kutatua matatizo.

Mogea (2022) anadokeza kwamba mtahini anapaswa kuandaa maswali ya mtihani yanayoweka mkazo kwenye tafakuri tunduizi kuliko kukariri tu. Hivyo basi, licha ya mtihani kuwa na maswali yanayowalazimu wanafunzi kukumbuka na kuchambua kile wanachojifunza darasani, mtihani unapaswa pia kuwa na maswali yanawasaidia wanafunzi kukuza tafakuri tunduizi kupitia tathmini, kupata maamuzi na kujenga hoja mpya ili ya kutatua matatizo (Negoescu, 2023). Hivyo basi, tumehamasika kuchambua mtihani wa mwaka uliofuata ili tuone hali ipoje ukilinganisha na mitihani tangulizi. Mtihani ufuataao ni wa mwaka wa 2022.

**SEHEMU YA III: FASIHI (Alama 30)**

17) Sanaa ni nini? **(alama 3)**
18) Nini maana ya fasihi. **(alama 3)**
19) Jadili umuhimu wa sanaa katika jamii. **(alama 4)**
20) Eleza maana ya methali zifuatazo: **(alama 5)**
    a) Leo ni leo asemaye kesho ni mwongo.
    b) Chelewa chelewa utamkuta mtoto si wako.
    c) Ndege aamkaye asubuhi hula wadudu watamu.
    d) Akili ni mali.
    e) Haraka haraka haina baraka.
21) Kila mtunzi wa mashairi au nyimbo ana uhuru katika utunzi. Jadili kuhusu uhuru huo ukitoa mifano. **(alama 6)**

2022-NESA *(National Examination and School Inspection Authority)* 028-Ukurasa 5 kwa 8

22) Fani na maudhui ni mambo yanayokamilishana katika kazi za fasihi. Kwa mifano thabiti jadili kauli hii. **(alama 4)**

23) Uhakiki wa kazi za fasihi si jambo la hivi karibuni. Eleza. **(alama 5)**

**Chanzo:** Data za Utafiti (2023)

Mtihani huu unaundwa na maswali mazuri kwa kuwa ni maswali ya msingi kuhusu fasihi. Kwa mfano, swali la 17 na 18 ni ya msingi kuhusu dhana ya sanaa na fasihi. Hii inatokana na kwamba huwezi kuzungumzia dhana yoyoye katika fasihi bila kuanzia kwenye maana ya sanaa na fasihi. Aidha, swali la 19 ni swali zuri kwa kuwa ni mwendelezo wa swali la 17 na 18.

Hata hivyo, ingekuwa bora swali la 19 likawa wazi zaidi na kumtaka mwanafunzi kujibu kwa kutoa mifano kutoka kazi za kifasihi au jamii yake. Swali lingeundwa namna hii ili kumsaidia mwanafunzi kuhusisha kile ambacho amesoma na maisha halisi. Vilevile, swali la 20 lina uhusiano wa karibu na swali lililoulizwa katika mitihani ya miaka ya 2018, 2019

na 2020-2021. Maelezo kuhusu swali hili yameshatolewa katika mitihani tangulizi iliyochambuliwa.

Swali la 21 ni swali zuri kwa sababu linamlazimu mwanafunzi kufanya mjadala (*kuchambua*). Hata hivyo, tuna maoni kwamba swali hili lingebainisha wazi kwamba mwanafunzi anatetea hoja zake kwa mifano kutoka mashairi tofauti aliyosoma. Kwa kufanya hivi, mwanafunzi angepata fursa ya kukuza stadi za tafakuri tunduizi ambazo ni kutathmini na kuunda. Isitoshe, swali la 22 lina uhusiano wa karibu na swali la 22 katika mtihani wa 2019. Kwa hiyo, tumeona kwamba haikuwa lazima tutoe maelezo tena ili kuepukana na uradidi.

Vilevile, swali la 23 ni zuri kwa kiwango cha kuelewa kwa kuwa linamlazimu mwanafunzi kukumbuka maarifa kuhusu nadharia. Pamoja na uzuri huu, tunapendekeza kuongezeka kwa maswali zaidi yanayowalazimisha wanafunzi kuhakiki kazi za kifasihi ili kuweka nadharia katika vitendo. Maswali kama haya, yangewasaidia wanafunzi kutoka kiwango cha kueleza *(eleza)* na kuwawezesha kukuza stadi za tafakuri tunduizi ambazo ni kuchambua na kutathmini (Krathwohl, 2001 katika Van Der Zanden, Denessen, Cillessen & Meijer, 2020). Mtihani wa taifa wa mwisho ambao ulichambuliwa ni ule wa mwaka wa masomo wa 2022-2023. Mtihani wenyewe uko hapo chini.

**SEHEMU YA III: FASIHI (ALAMA 30)**

16) Sanaa ni nini? **(alama 2)**

17) Hurafa na hekaya zote ni mojawapo ya aina za hadithi simulizi zenye umuhimu katika jamii. Toa tofauti zilizopo kati ya hadithi hizi. **(alama 5)**

18) Kamilisha methali zifuatazo ili ziwe na maana kamili: **(alama 5)**

a) Yaliyopita si ndwele.................
b) Mtoto umleavyo ....................................................
c) ................................. huumiza matumbo
d) Mchelea mwana kulia ..........................
e) ...................................... hufunzwa na ulimwengu.

19) Taja kisha ueleze hoja tatu kuhusu umuhimu wa vitendawili katika jamii husika. **(alama 6)**

*2022-2023-NESA (National Examination and School Inspection Authority)* 027 ukurasa wa 6 kati ya 8

CS CamScanner

20) Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayohusika:

**Magawi**

1. Farakano za hewani, zenye kuzusha mikasa,
Wema ukiwa moyoni, kweli hutazitomasa,
Utaziacha njiani, ziende zinakopasa,
Ugomvi, usengenyi, adui za mtu mwema.

2. Ukarimu maishani, upole, utii hasa,
Mambo haya duniani, yazishinda hata pesa,
Wema kitu cha thamani, toka jana hadi sasa,
Mtu aliye na wema, anazo busara nyingi

**Maswali:**

a) Andika vina vya kati na vina vya mwisho **(alama 2)**
b) Andika idadi ya mizani iliyomo katika kila mshororo wa ubeti wa kwanza. **(alama 2)**
c) Ni beti ngapi zinazounda shairi hili. **(alama 2)**

21) Eleza kinagaubaga aina za wahusika wafuatao wanaopatikana katika riwaya:

a) Wahusika wakuu **(alama 2)**
b) Wahusika wasaidizi **(alama 2)**
c) Wahusika wadogo **(alama 2)**

**Chanzo:** Data za Utafiti (2023)

Maswali yanayounda mtihani huu ni mazuri kwa kuwa yanazingatia maudhui muhimu ya fasihi ambayo ni msingi wa kukuza tafakuri tunduizi kwa mwanafunzi. Pamoja na hayo, kuna maswali yanayohusiana na mtihani tangulizi pia. Kwa mfano, kuna mfanano uliopo kati ya swali la 16 na swali la 17 la mtihani wa 2022. Maelezo kuhusu maswali haya yameshatolewa vilevile.

Swali la 17 ni swali zuri kwa kuwa linamlazimu mwanafunzi kutofautisha *hurafa* na *hekaya* ambazo ni dhana za msingi pia katika fasihi. Pamoja na uzuri wa swali hili, tunaona kwamba lingewalazimu wanafunzi kutofautisha dhana hizi kwa kutumia mifano kutoka *hekaya* na *hurafa* ambazo wamesoma au kusikiliza. Kwa kufanya hivi, wanafunzi wangekuwa na uwezo wa kutetea majibu yao wakiwa na uthibitisho kutoka kazi hizo.

Swali la 18 ni swali ambalo linawalazimu wanafunzi kujaza methali. Kwa maneno mengine, wanafunzi wanahitajika tu kukumbuka kile walichosoma darasani ili kujibu swali hili. Kwa maoni yetu, tunaona kwamba kumeongezewa swali linalowalazimu wanafunzi kufafanua methali husika. Hii ingewasaidia wanafunzi kutetea na kujenga hoja wanazozitoa kwa mifano kutoka jamii yao au kazi za kifasihi. Kwa kufanya hivi, wanafunzi wangepata fursa ya kuhusiha methali na maisha yao kila siku.

Pia, swali la 19 ni zuri kwa kuwa linawataka wanafunzi kutaja na kueleza (*kuelewa*) umuhimu wa vitendawili katika jamii. Hata hivyo, swali hili lingebainisha wazi kwamba wanafunzi wanapaswa kutetea hoja zao kwa mifano kutoka maisha ya kila siku katika jamii au kazi za kifasihi. Hii ingewapa wanafunzi fursa ya kuhusisha vitendawili na maisha halisi ya kila siku. Vilevile, swali la 20 ni swali zuri kwa kiwango cha kuchambua. Maelezo kuhusu swali hili yametolewa katika uchambuzi wa mtihani wa mwaka wa 2018 na 2021-2022. Hatuna haja ya kuyarudia.

Hali kadhalika, swali la 21 linamtaka mwanafunzi kueleza (*kuelewa*) aina za wahusika. Hii ina maana kwamba mwanafunzi anahitajika kuwa anakumbuka aina za wahusika ili aweze kujibu swali kwa ukamilifu. Pamoja na uzuri huu, ingefaa zaidi wanafunzi kuulizwa kubainisha aina za wahusika wanaopatikana katika kazi za kifasihi walizosoma na kueleza sababu za kuridhishwa au kutoridhishwa na tabia zao. Swali kama hili lingetoa fursa sio tu kutetea hoja zao kwa mifano bali pia kuhusisha tabia za wahusika na zao wenyewe au tabia za watu wengine katika jamii. Hii ingewapa wanafunzi fursa ya kuweza kujirekebisha au kuendeleza tabia hizo pia.

Kwa ujumla, maswali ya mitihani iliyochambuliwa ni mazuri kwa sababu yanazingatia maarifa ya msingi kuhusu fasihi. Aidha, ngazi za chini za grafu ya Taksonomia ya Bloom ambazo ni *kukumbuka, kuelewa* na *kutumia* zimezingatiwa kwa ufanisi. Kuzingatiwa kwa ngazi hizi kunatoa fursa kwa wanafunzi kukuza stadi za tafakuri tunduizi ambazo ni kuchambua, kutathmini na kuunda. Hii pia inatetewa na mmojawapo wa mhimili wa Nadharia ya Taksonomia ya Bloom usemao kwamba ufundishaji na tathmini unapaswa kujumuisha ngazi zote za tathmini kutoka ngazi chini hadi ngazi za juu.

Licha ya hayo, tumeona kwamba kuna maswali yanayohitaji kuboreshwa ili yawasaidie wanafunzi kukuza stadi zote za tafakuri tunduizi kama inavyobainishwa. Aidha, baadhi ya maswali ya mitihani iliyochambuliwa yanafafana kimuundo. Vilevile, alama zinazopewa kipengele cha fasihi zinatofautiana kutoka mtihani mmoja hadi mwingine. Kuna mitihani ambayo fasihi ilipewa alama 25 na kwingine alama 30. Hali hii ni tofauti na utaratibu unaopendekezwa katika muhtasari wa Kiswahili. Mhutasari huu unapendekeza kwamba fasihi inapaswa kutathminiwa kwa alama asilimia 40. Hii ina maana kwamba kipengele cha fasihi kinapaswa kupewa alama 40 katika mtihani (REB, 2015a). Haya yote yametuhamasisha kupendekeza mikakati ya kutathmini somo la Kiswahili kwa kujumuisha stadi za tafakuri tunduizi.

**Mikakati ya Kuandaa Tathmini Inayojumuisha Tafakuri Tunduizi**

Kutokana kutojumuisha stadi za tafakuri tunduizi kwa ufanisi wake katika mitihani ya taifa ya somo la Kiswahili, tumeona kwamba ni muhimu kupendekeza mikakati mbalimbali inayoweza kutumiwa wakati wa kuandaa tathmini. Mikakati hii pia inaweza kutumiwa kwa kiwango cha taifa na kile cha shule au wilaya. Hii inatokana na kwamba walimu wa Kiswahili kwa kiwango cha shule walionekana kuandaa maswali ya tathmini yanayomtaka mwanafunzi kukariri kile anachokifunza tu kuliko kumlazimu kukihusisha na hali halisi ya maisha (Tuyishimire & Mlaga, 2023). Hivyo basi, mikakati hii ikizingatiwa, itasaidia kuandaa tathmini inayozingatia tafakuri tunduizi na hivyo itatoa fursa ya kumuandaa mwanafunzi mwenye uwezo wa kutatua matatizo ya kimaisha kwa ufanisi vilevile. Mikakati hiyo ni hii ifuatayo:

Mosi, kuchunguza malengo ya somo. Kabla ya kuandaa tathmini, mwalimu/ mtahini anapaswa kuchunguza malengo ya somo kama yanavyojitokeza katika silabasi. Hii itamsaidia kuelewa nini wanafunzi wanatarajiwa kufanya baada ya kiwango husika (REB, 2015a). Kwa kufanya hivi, mtahini ataweza kutambua aina ya maswali anayoweza kuandaa kulingana na melengo yanayotarajiwa.

Pili, mtahini anapaswa kutengeneza jedwali la mgawanyo wa maswali kabla ya kuandaa mtihani. Jedwali hili litamsaidia kutambua idadi ya maswali anayopaswa kuandaliwa na uzito wa kila swali kwa kurejelea grafu ya Taksonomia ya Bloom. Kwa hiyo, mtahini anapaswa kuhakikisha kwamba ametumia vitenzi tendaji vinavyoonesha wazi nini mwanafunzi ataweza kufanya kama matokeo ya ujifunzaji.

Tatu, mtahini anapoandaa tathmini anapaswa kuhakikisha kwamba ananzia kwenye kile mwanafunzi anakumbuka hadi kile anachoweza kuunda mwenyewe kama matokeo ya ujifunzaji. Kwa maneno mengine, mtahini anatarajiwa kutathmini kuanzia kwenye ngazi za chini ambazo ni *kukumbuka, kuelewa* na *kutumia* hadi ngazi za juu za tafakuri tunduizi ambazo ni *kuchambua, kutathmini* na *kuunda* (Krathwohl, 2001 katika Van Der Zanden wenzake, 2020).

Nne, ni wajibu wa mtahini kuhakikisha kwamba maswali anayoyatoa kwa wanafunzi ikiwa yanahusiana na muktadha halisi wa utatuzi wa matatizo (Lai, 2009). Hii ina maana kwamba maswali ya tathmini yanapaswa kutengenezwa kwa namna ya kuwalazimu wanafunzi kubuni mawazo mapya au kitu fulani kama njia ya mojawapo ya kutatua tatizo lililopo. Kwa mfano, wanafunzi wanaweza kutunga kazi mbalimbali za kifasihi kwa ajili ya kutatua matatizo mbalimbali yaliyopo katika jamii au kama kama njia mojawapo wa kujiajiri.

Tano, inafaa zaidi kutoa na kubainisha kazi za kifasihi zinazoweza kutumiwa katika ufundishaji na ujifunzaji. Kupatikana kazi hizi kutasaidia walimu kuwashirikisha wanafunzi katika usomaji wake. Aidha, wanafunzi wataweza kujibu maswali mbalimbali ya mitihani kwa kurejelea kile ambacho wamesoma au kusikiliza.Vilevile, usomaji kazi hizi unaweza kuwa kichocheo kizuri kwa wanafunzi kuweza kutunga kazi zao kama njia mojawapo ya kujiajiri. Isitoshe, tunapendekeza kufanyika kwa tafiti zaidi kuhusu ufundishaji wa tafakuri tunduizi katika viwango mbalimbali vya elimu.

**Hitimisho**

Makala hii imejadili ujumuishaji wa stadi za tafakuri tunduizi katika mitihani ya taifa ya Kiswahili ya shule za sekondari nchini Rwanda. Pia inapendekeza mikakati ya kuandaa tathmini inayojumuisha stadi za tafakuri tunduizi. Kutokana na mitihani tuliyochanganua, tumebaini kwamba mtihani ni mizuri kutokana na kwamba inazingatia grafu ya Taksonomia ya Bloom ambapo maswali mengi yanapaswa kuweka mkazo kwenye ngazi cha chini ambazo ni *kukumbuka, kuelewa* na *kutumia*. Hata hivyo, baadhi ya maswali yanayounda mitihani teule yanafafana kimuundo. Tumeona pia kwamba alama zinazotolewa katika kipengele cha fasihi ni tofauti na zile zinazopendekezwa katika silabasi. Vilevile, stadi za tafakuri tunduizi hazikujumuishwa kwa ufanisi katika mtihani hii kutokana na kwamba baadhi ya maswali hayakuandaliwa kwa kuwalazimisha wanafunzi kuzalisha hoja mpya kutokana na ujuzi walionao.

Kwa hiyo, tumependekeza mikakati inayoweza kufuatiwa wakati wa kuandaa tathmini katika somo la Kiswahili. Mikakati hii inaweza kutekelezwa sio tu katika kiwango cha taifa bali pia katika kiwango cha shule na wilaya. Baadhi ya mikakati hiyo ni pamoja na kuzingatia malengo na mahitaji ya mwanafunzi, kuhakikisha kuwa mwanafunzi anaweza kuzalisha mawazo mapya kama matokeo ya ujifunzaji na kufanyika kwa tafiti zaidi kuhusu tathmini ya tafakuri tunduizi.

**Declaration of conflicting interests**

The author (s) declared that there is not any conflict of interest (s) with respect to the research, authorship and/or publication of this paper.

**Funding**

The author (s) declared that reseach was privately funded.

**Marejeleo**

Alsaleh, N. J. (2020). Teaching Critical Thinking Skills. *The Turkish Online Journal of Educational Technology*, 19(1): 21–39. https://doi.org/10.4324/9780429342042.

Belecina, R. R. & Ocampo, J.M. (2018). Effecting Change on Students' Critical Thinking Problem Solving. *International Journal for Educational Studies*, 10(2): 109-117.

Chandio, M. T., Pandhiani, S. M. & Iqbal, R. (2016). Bloom's Taxonomy: Improving Assessment and Teaching-Learning Process. *Journal of Education and Educational Development*, 3(2): 203-221.

Lai, Y. K. (2009). Assessing Students' Critical Thinking Performance: Urging for Measurements Using Multi-Response Format. *Journal of Thinking Skills and Creativity*, 4(1): 70-76.

Mogea, T. (2022). Students' Critical Thinking Ability in English Teaching and Learning. *Jurnal Jupensi,* 2(3): 157-171.

Ndayambaje, I., Kamanzi, F., Murereyimana, M. S. B., Ntahomvukiye, C. & Otara, A. S. (2023). Paths to School Reopening after Covid-19 in Rwanda: School Leaders' Self-Reported Roles, Strategies Adopted and Perceptions on the Role of Professional Learning Communities. *Rwandan Journal of Education,* 7(1): 90-102.

Negoescu, A. G. (2023). The Value of Critical Thinking in the Language Classroom. *Land Forces Academy Review*, 4(112): 303-308.

NESA. (2022). *Subject Paper Tandards for the end-of Second Term, 2021-2022 School Year*. Kigali: NESA.

Ngonyani, D. (2005). Vitendawili vya Kiswahili: Usambamba wake na Dhima yake katika Jamii. *Swahili Forum*, 12: 121-132.

Nsengimana, V. (2021). Implementation of Competence-Based Curriculum in Rwanda: Opportunities and Challenges. *Rwandan Journal of Education*, 5(1): 129-138.

REB. (2015) *Muhtasari wa Somo la Kiswahili Kidato cha 4-6: Mchepuo wa Lugha.* Kigali: REB.

REB. (2015a). *Teacher Training Manual: Roll Out of the Competence-Based Curriculum.* Kigali: REB.

Rezaei, S., Derakhshan, A. & Bagherkazemi, M. (2011). Critical thinking in Language Education. *Journal of Language Teaching and Research*, 2(4):769-777. Doi:10.4304/jltr.2.4.769-777.

Schendel, R. (2015). Critical thinking at Rwanda's Public Universities: Emerging Evidence of a Crucial Development Priority. *International Journal of Educational Development*, 42: 96-105.

Shirkhani, S. & Fahim, M. (2011). Enhancing Critical Thinking in Foreign Language Learners. *Procedia - Social and Behavioral Sciences*, 29:111–115.

Sidhu, G.K., Fook, C.Y., & Kaur, S. (2010). Instructional Practices in Teaching Literature: Observations of ESL Classrooms in Malaysia. *English Language Teaching*, 3(2): 54-63.

Silverman, D. & Marvasti, A. (2008). *Doing Qualitative Research: A Comprehensive Guide*. Los Angeles na London: Sage Publications.

Tung, C. A. & Chang, S. Y. (2009). Developing Critical Thinking through Literature Reading. Feng. *Chia Journal of Humanities and Social Sciences,* 19(1): 287-317.

Tuyishimire, L. & Mlaga, W. (2021). Matumizi wa Fasihi katika Ukuzaji wa Tafakuri Tunduizi. Jarida la *CHALUFAKITA* , 3(1): 93-120.

Tuyishimire, L. & Mlaga, W. (2023). Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la Kiswahili Unaozingatia Stadi ya Tafakuri Tunduizi: Mifano Kutoka Shule Teule za Sekondari Wilayani Nyagatare. *Jarida la Mulika.* 42 (2):164-183. DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na42t2.2

Van Der Zanden, P. J.A.C, Denessen, E., Cillessen, A. H.N. & Meijer, P. C. (2020). Fostering Critical Thinking Skills in Secondary Education to Prepare Students for University: Teacher Perceptions and Practices. *Research in Post-Compulsory Education,* 25(4):394-419. https://doi.org/10.1080/13596748.2020.1846313.

## Author Biographies

**Laurien Tuyishimire** is an Assistant Lecturer in the Department of Humanities and Language Education in Kiswahili Section, University of Rwanda College of Education (UR-CE). His resarch interests are Kiswahili literature and linguistics, integration of 21$^{st}$ century skills in Kiswahili teaching and learning, and language education. His recent publications are: Matumizi ya Fasihi katika Ukuzaji wa Tafakuri Tunduizi (CHALUFAKITA, 2021; with W. Mlaga); Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la Kiswahili Unaozingatia Stadi ya Tafakuri Tunduizi: Mifano kutoka Shule Teule za Sekondari Wilayani Nyagatare (Mulika, 2023; with W. Mlaga) and Riwaya za Euphrase Kezilahabi kama Nyenzo Mwafaka za Ukuzaji wa Stadi ya Tafakuri Tunduizi: Mfano wa Nagona na Mzingile (Kiswahili Journal, 2023; with W. Mlaga).

**Donard Bikorimana** is an Assistant Lecturer at Kibogora Polytechinic University, Faculty of Education and Department of Languages. His research interests are in the areas of

education, teaching, and learning of foreign and second languages, literature, and linguistic analysis. He recently published Ufundishaji wa Kiswahili kama Lugha ya Pili kupitia Fasihi (Nuru ya Kiswahili, 2023), Assessing the Use of ICT in Teaching and Learning a Foreign Language in Rwandan Schools (ELS Journal on Interdisciplinary Studies in Humanities, 2023; with, P. Murwanashyaka) and Teachers' Extrinsic Motivation on Quality Education in Nyamasheke District, Rwanda (East African Journal of Education Studies, 2024; with P. Murwanashyaka, V. Berabose, L. Tuyishimire, J. B. Turatsinze & G. Tuyizere).